**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

# TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIKATABA YA HIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA

**JANUARI, 2024**

**TAARIFA FUPI ZA UTEKELEZAJI WA MIKATABA YA HIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA KWA MWAKA 2023/2024**

## 1.0 UTANGULIZI

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais (OMR) inatekeleza na kuratibu shughuli ya hifadhi na usimamizi wa Mazingira kwa manufaa mapana ya Kitaifa kwa Kizazi hiki na kizazi kijacho. Utekelezaji wa shughuli za Hifadhi na usimamizi wa Mazingira zinafanywa kwa mwongozo wa Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021 na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira sura Namba 191.

Aidha, katika utekelezaji wa shughuli hizi, Serikali imekuwa ikitekeleza majukumu yake Kitaifa na Kimataifa ambapo katika nyanja za Kimataifa Serikali ni mwanachama wa Mikataba mbalimbali ya Kimataifa ya Mazingira (*Multilateral Environmental Agreements – MEAs*) na Kikanda.

Taarifa hii imejumuisha maelezo mafupi ya utekelezaji wa shughuli chini ya Mikataba 12.

### 1. Orodha ya Mikataba

#### 1.1. Mikataba inayohusika na masuala ya Mabadiliko ya Tabianchi

1.1.1. Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi (United Nations Framework Convention on Climate Change - UNFCCC)

1.1.2. Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Kupambana na Kuenea Kwa Hali ya Jangwa (*United Nations Convention to Combat Desertification – UNCCD*).

#### 1.2. Mikataba inayohusika na masuala ya Hifadhi ya Bioanuai

1.2.1. Mkataba wa Ramsar wa Usimamizi wa Maeneo ya Ardhi Oevu (*Ramsar Convetion on Wetlands*)

1.2.2. Mkataba Wa Umoja wa Mataifa wa Hifadhi ya Bioanuai *(United Nations Convention on Biological Diversity-CBD)*

1.2.3. Mkataba wa Usimamizi Endelevu wa Ziwa Tanganyika *(The Convention on The Sustainable Management of Lake Tanganyika)*

1.2.4. Mkataba wa Nairobi kuhusu Hifadhi, Usimamizi na Uendelezaji wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani ya Magharibi ya Bahari ya Hindi

(*Convention for the Protection, Management, and Development of the Marine and Coastal Environment of the Eastern African Region)*

*1.3.* **Mikataba inayohusika na masuala ya udhibiti wa Uchafuzi wa Mazingira**

1.3.1. Mkataba wa Vienna Unaohusu Hifadhi ya Tabaka La Ozoni na Itifaki ya Montreal Kuhusu Kemikali Zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni.

1.3.2. Mkataba wa Minamata Kuhusu Usimamizi wa Zebaki

1.3.3. Mkataba wa Basel Kuhusu Udhibiti wa Usafirishaji wa Taka Hatarishi Baina ya Nchi na Nchi na Utupaji Wake.

1.3.4. Mkataba wa Stockholm Kuhusu Udhibiti wa Kemikali Zinazodumu Kwenye Mazingira Kwa Muda Mrefu.

1.3.5. Mkataba wa Bamako Kuhusu Udhibiti wa Taka Hatarishi Bara la Afrika

1.3.6. Mkataba wa Rotterdam upashanaji taarifa kuhusu baadhi ya kemikali hatarishi za viwandani na viuatilifu katika biashara ya kimataifa

## 2.0 UTEKELEZAJI WA MIKATABA

| **1. MKATABA WA UMOJA WA MATAIFA WA MABADILIKO YA TABIANCHI (UNITED NATIONS FRAMEWORK CONVENTION ON CLIMATE CHANGE - UNFCCC)** | | |
|---|---|---|
| 1.1 | **Utangulizi** | **1.1 Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi**(***United Nations Framework Convention on Climate Change - UNFCCC)***. Mkataba huu ulianzishwa mwaka 1992 wakati wa kilele cha Mkutano wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mazingira na Maendeleo uliofanyika Rio De Janeiro, Brazil. Mkataba huu una jumla ya Nchi Wanachama **198**. Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliridhia mkataba huu mwezi Aprili, 1996. Mkataba ulianza kufanyakazi mwaka 1994. Aidha, Mkataba huu una mikataba midogo, ikiwemo Itifaki ya Kyoto na Makubaliano ya Paris ili kuwezesha utekelezaji wa Mkataba.<br><br>**1.2 Itifaki ya Kyoto (*The Kyoto Protocol*)**<br>Itifaki ya Kyoto ilianzishwa mwaka 1997. Itifaki hii ina jumla ya Nchi Wanachama **192**. Itifaki ilianza kufanyakazi mwaka 2005. Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliridhia Itifaki ya Kyoto mwezi Agosti, 2002.<br><br>**1.3 Makubaliano ya Paris (*The Paris Agreement*)**<br>Makubaliano ya Paris yalianzishwa mwaka 2015 mjini Paris, Ufaransa |

| | | |
|---|---|---|
| | | wakati wa mkutano 21 wa Nchi Wanachama wa Umoja wa Mataifa wa Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi. Makubaliano haya yana jumla ya Nchi Wanachama **195** na yalianza kufanya kazi mwaka 2016. Tanzania iliridhia Makubaliano ya Paris mwezi Mei, 2018. |
| 1.2 | **Lengo la Mkataba, Itifaki na Makubaliano ya Paris** | 1.2 ***Lengo la Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi*** ni Kuzuia ongezeko la gesijoto na athari zitokanazo na mabadiliko ya tabianchi kwenye mifumo ya ikolojia ya Dunia ili kuhakikisha maendeleo endelevu duniani.<br>1.3 ***Lengo la Itifaki ya Kyoto*** ni kuzibana kisheria nchi zinazozalisha gesijoto ili kupunguza uzalishaji wake kwa kuwekewa shabaha maalumu ya kiwango cha kupunguza gesijoto kwa asilimia 5 ilikilinganishwa na uzalishaji wake wa mwaka 1990.<br>1.4 ***Lengo la Makubaliano ya Paris*** ni kushirikisha nchi zote wanachama katika juhudi za kushughulikia mabadiliko ya tabianchi hasa upunguzaji wa gesijoto kwa angalau chini nyuzi joto 2 au 1.5 na kusaidia nchi zinazoendelea kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi na kuchochea maendeleo endelevu. Utekelezaji unazingatia misingi ya usawa, uwezo na hali ya uchumi wa nchi husika. |
| 1.3 | **Shughuli zinazotekelezwa na Mkataba** | **1.4 *Miradi inayotekelezwa:***<br><br>Miradi inayotekelezwa chini ya Mkataba, Itifaki ya Kyoto na Makubaliano ya Paris ni pamoja na:<br><br>i. Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya tabianchi kwa kutumia Mifumo Ikolojia Vijijini (2017-2023). Lengo ni Kuongeza uhimilivu kwa athari za mabadiliko ya tabianchi katika jamii za vijijini nchini, kwa kuimarisha mifumo ikolojia.<br><br>ii. Mradi wa Majaribio wa Kikanda wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi katika Bonde la Ziwa Victoria (Wilaya ya Magu, Mwanza) (2019-2023). Lengo ni kuwezesha jamii zinazozunguka Bonde la Ziwa Victoria kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi.<br><br>iii. Shughuli Wezeshi ya Kuandaa Taarifa ya Tatu ya Utekelezaji wa Mkataba (2022-2025); na Shughuli Wezeshi ya kuandaa Taarifa kuhusu upunguzaji wa gesijoto nchini (2022-2024). Lengo la mradi huu ni kuandaa taarifa za utekelezaji wa Mkataba wa Mabadiliko ya tabianchi, Itifaki ya Kyoto pamoja na Mchango wa Taifa wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi chini ya Makubaliano ya Paris, kulingana na matakwa ya mkataba. |

| | | |
|---|---|---|
| | | iv. Mradi wa ujenzi wa Ukuta wa kuzuia mawimbi ya bahari katika maeneo ya Mikindani (Mtwara) na Sipwese, Pemba (Zanzibar). Lengo la mradi huu ni kuwezesha maeneo husika kuhimili athari za kuongezeka kwa maji ya bahari na kuzuia mmomonyoko wa udongo katika ukanda wa Pwani katika fukwe za mikoa ya Mtwara na Pemba.<br><br>v. Mradi wa Kujenga Uwezo wa Taasisi ili kupunguza uzalishaji wa kaboni unaosababishwa na ukataji miti na uharibifu wa misitu (2020-2023). Lengo la mradi huu ni kuwezesha Tanzania kushiriki kikamilifu katika shughuli za upunguzaji wa gesijoto na kunufaika na shughuli hizo.<br><br>vi. Shughuli Wezeshi ya Kuandaa Mpango wa Taifa wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi (*National Adaptation Plan - NAP*) (2022- 2026). Lengo la mradi ni kuimarisha uwezo wa taifa kuhimili mabadiliko ya tabianchi.<br><br>vii. Mradi wa majaribio wa kuwezesha kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi katika ngazi ya jamii (*Local Climate Adaptive Living – LoCAL*) unaofadhiliwa na Mfuko wa Umoja wa Mataifa wa Kuendeleza Mitaji (*UN Capital Development Fund – UNCDF*). Lengo la mradi huu ni kusaidia halmashauri utekelezaji na usimamizi wa mradi wa kuwezesha kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi katika ngazi ya jamii.<br><br>viii. Mradi wa kuhimili mabadiliko ya tabianchi Simiyu (Simiyu Water Resilient). Lengo la mradi huu ni kuwezesha upatikanaji wa maji katika mkoa wa Simiyu ili kusaidia kujenga uwezo wa kuhimili mabadiliko ya tabianchi. Mradi unafadhiliwa na Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi (Green Climate Fund) kupitia Benki ya KfW ya Ujerumani.<br><br>ix. Mradi wa kuhimili madailiko ya tabianchi inayofadhiliwa na mfuko wa kuhimili mabadiliko ya tabianchi kupitia NEMC. Miradi hiyo ni: *Enhancing Climate Change Adaptation for Agro-Pastoral Communities in Kongwa District (USD 1,200,000); Strategic Water Harvesting Technologies for Enhancing Resilience to Climate Change in Rural Communities in Semi-Arid Areas of Tanzania (SWAHAT) in Singida, Tabora and Dodoma Regions; Enhancing Climate Change Resilience of Coastal Communities of Zanzibar (USD 1,000,000) na Bunda Climate Resilient and Adaptation Project (USD 1,400,000)***.** |

| | | |
|---|---|---|
| | | x. Mradi wa kujenga uwezo katika sekta ya Kilimo unaotekelezwa na Benki ya CRDB kwa ufadhili wa GCF.<br><br>**1.5 *Shughuli zingine zinazotekelezwa:***<br><br>xi. Kuandaa miradi ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi na kupunguza gesijoto kwa ajili ya kuwasilisha Mfuko wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi na wafadhili wengine.<br>xii. Kuandaa Msimamo wa nchi na kuratibu ushiriki wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania katika mikutano ya nchi wanachama wa mkataba wa Mabadiliko ya tabianchi, Itifaki ya Kyoto na Makubaliano ya Paris.<br>xiii. Kuandaa andiko la kuwezesha ushirikiano kati ya Tanzania na Norway katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi<br>xiv. Kusimamia na kuwezesha utekelezaji wa miradi ya biashara ya Kaboni kwa mujibu wa Kanuni na Mwongozo wa Udhibiti na Usimamizi wa biashara ya Kaboni, 2022 ambapo miradi 35 imewasilisha maombi ya kuomba idhini ya utekelezaji hadi Desemba 2023.<br>xv. Kufanya mapitio ya Mwongozo wa Udhibiti na Usimamizi wa Biashara ya Kaboni, 2022.<br>xvi. Kupitia maombi ya miradi ya mabadiliko ya tabianchi inayoomba idhini ya ufadhili na *ithibati* chini ya Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi na (*Green Climate Fund - GCF*)<br>xvii. Kuandaa mpango wa utekelezaji wa mradi wa kuhimili mabadiliko ya tabianchi katika mkoa wa Kigoma wenye thamani ya Dola za Marekani milioni 19 chini ya ufadhili wa Mfuko wa Kuhimili Mbadiliko ya Tabianchi kupitia UNEP.<br>xviii. Kuandaa mpango wa utekelezaji wa Mradi wa Kujenga uwezo wa Taifa katika kutekeleza Ibara ya 6 ya Makubaliano ya Paris kuhusu Biashara ya Kaboni wenye thamni ya Dola 250,000 chini ya ufadhili wa Umoja wa Ulaya kupitia UNEP.<br>xix. Kuendelea na maandalizi na utekelezaji wa miradi chini ya mkataba huu kama ilivyobainishwa katika taarifa za miradi husika. |
| 1.4 | **Mafanikio** | i. Upatikanaji wa fedha za kutekeleza miradi kutoka mifuko ya kimataifa na wadau wa maendeleo<br>ii. Kuimarisha ushirikiano na jumuiya ya kimataifa katika nyanja za utafiti na uendelezaji wa teknolojia za mabadiliko ya tabianchi. |

| | | |
|---|---|---|
| | | iii. Taasisi ya Tanzania kupata ithibati katika mifuko ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi na mfuko wa Mabdiliko ya tabianchi<br>iv. Utekelezaji wa miradi ya mabadiliko ya tabianchi kuchangia katika jitihada ya maendeleo na upatikaji wa huduma nchini<br>v. Kuongeza upatikanaji wa fedha za kigeni kutokana na fedha za miradi zinazoletwa nchini<br>vi. Kuongeza uelewa kwa jamii kuhusu mabadiliko ya tabianchi na athari zake<br>vii. Upatikanaji wa fursa za mafunzo kwa wanafunzi wa ngazi mbalimbali kuhusu mbadiliko ya tabianchi |
| 1.5 | **Changamoto** | **1.6.1 *Changamoto za kitaifa***<br>i. Gharama kubwa za miradi ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.<br>ii. Uelewa mdogo wa jamii kuhusu mabadiliko ya tabianchi na fursa za biashara ya kaboni.<br>iii. Teknolojia za kubaini mapema athari za mabadiliko ya tabianchi na kuweka maandalizi stahiki.<br>iv. Mchakato mrefu na gharama kubwa za kuandaa miradi ya biashara ya Kaboni.<br>v. Uhaba wa watalaam wa kuandaa miradi kulingana na matakwa ya Mifuko ya Mabadiliko ya tabianchi.<br>vi. Uhaba wa vifaa vya kufuatilia mabadiliko y tabianchi.<br>vii. Ucheleweshaji wa fedha kutoka kwa baadhi ya wafadhili<br><br>***1.6.2 Changamoto za kimataifa***<br>i. Uzalishaji wa gesijoto duniani unazidi kuongezeka na kuzidisha athari za mabadiliko ya tabianchi hususan ukame, mafuriko na kujaa kwa maji ya bahari.<br>ii. Nchi zilizoendelea kutotimiza ahadi yake ya kutoa fedha na teknolojia kwa mujibu wa Mkataba, Itifaki ya Kyoto na Makubaliano ya Paris.<br>iii. Sera ya kimataifa zinazoshinikiza kauchana na matumizi ya rasilimali zinazoweza kuchangia katika maendeleo<br>iv. Utaratibu mrefu wa upatikanaji wa fedha za mabadiliko ya tabianchi |
| 1.6 | **Ushiriki wa Mikutano na matarajio** | 1.7.1 Mikutano<br>Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hushiriki katika mikutano chini ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa ambayo hufanyika kila mwaka katika ngazi za kimataifa na kikanda. Mikutano ambayo Jamhuri ya |

| | | |
|---|---|---|
| | | Muungano imeshiriki kwa mwaka 2023 ni:<br>i. Mkutano wa Kamati za Watalaam kuhusu sayansi, ushauri na utekelezaji wa Mkataba ulifanyika mwezi 5-15 Juni 2023, Bonn, Ujerumani.<br>ii. Mkutano wa watalaamu (Expert Working Group (EWG) Meeting) kuhusu mabadiliko ya tabianchi na uhamaji ulifanyika mwezi Mei 2023, Kampala, Uganda.<br>iii. Mkutano wa Mfuko wa Mabdiliko ya Tabianchi ulifanyika tarehe 6-9 Novemba Winhoek, Namibia.<br>iv. Mkutano wa Watalaam wa Kuandaa Mipango ya Taifa ya Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi, 27-30 Machi 2023, Santiago, Chile.<br>v. Mkutano wa Maandalizi ya ushiriki kwa nchi za Afrika ulifanyika Nairobi tarehe 3-9 Septemba 2023<br>vi. Mkutano wa Nchi zinanzoendelea zenye Uchumi wa chini ulifanyika tarehe 26-29 Septemba 2023, Dakar, Senegal<br>vii. Mkutano Kamati ya watalaamu kuhusu mabadiliko ya tabianchi uloifanyika Bangkok, Thailand, 14-18 July 2023<br>viii. Mkutano wa watalaamu kuhusu upunguzaji wa gesijoto ulifanyika tarehe 15-17 October 2023, Abu Dhabi 2023<br>ix. Mkutano wa Watalaam wa Afrika kuhusu Mabadiliko yaTabianchi ulifanyika Addis Ababa, tarehe 14-18 Agosti 2023<br>x. Mkutano wa Kamati ya Watalaam kuhusu kujenga uwezo wa Kukabliana na mbadiliko ya tabianchi ulifanyika tarehe 15-18 Juni 2023, Bonn Ujerumani<br>xi. Mkutano wa Watalaamu kuhusu mchakato wa kuanzisha lengo la pamoja na kukusanya fedha za mabadiliko ya tabianchi ulifanyika tarehe 2-6 Oktoba 2023, Geniva, Uswis.<br>xii. Mkutano wa Maandalizi ya kushiriki COP 28 kwa nchi za Afrika Mashariki ulifanyika mwezi 11-14 Novemba 2023, Kigali, Rwanda<br>xiii. Mkutano wa Nchi Wanachama wa Mabadiliko ya Tabianchi. Mkutano wa 28 ulifanyika Dubai, UAE, tarehe 30 Novemba – 12 Desemba 2023.<br><br>**1.7.2 Fursa na matarajio**<br><br>• Upatikanaji wa fedha za kutekeleza miradi kutoka mifuko ya kimataifa na wadau wa maendeleo<br>• Kuimarisha ushirikiano na jumuiya ya kimataifa katika nyanja za utafiti na uendelezaji wa teknolojia za mabadiliko ya tabianchi<br>• Kuendeleza majadaliano na taasisi za kimataifa kuhusu |

| | | |
|---|---|---|
| | | ufadhili wa miradi na upatikanaji wa ithibati katika mifuko ya ya mabadiliko ya tabianchi<br>• Kupata ujuzi na kubadilishana uzoefu wa jitihada za kukabliana na mabadiliko ya tabianchi.<br>• Kupanua wigo wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya miradi ya kukabliana na mabadiliko ya tabianchi.<br>• Kufuatilia kwa karibu miradi na changamoto za upatikanaji wa ithibathi<br>• Kuhakikisha maslahi ya Tanzania yanajumuiswa katika maazimiao ya mkutano<br>• Kutangaza fursa za uwekezaji kwa wadau mbalimbali wa mabadiliko ya tabianchi |
| 1.7 | **Hatua zinazochukuliwa** | i. Kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya mabadiliko ya tabianchi na athari zake.<br>ii. Kujenga uwezo na uelewa wa jamii kuhusu fursa za biashara ya kaboni.<br>iii. Kuendelea kushirikiana na jumuiya ya kimataifa katika jitihada za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.<br>iv. Kufuatilia utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Taifa (2022-2032); Mchango wa Taifa wa Mabadiliko ya Tabianchi; na Mkakati wa Taifa wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi.<br>v. Kuendelea kuandaa maandiko ya miradi kuwezesha utekelezaji wa Mkataba husika.<br>vi. Kushiriki katika mikutano na majadiliano ya kitaifa kwa lengo la kutafuta ufumbuzi wa changamoto za mabadiliko ya tabianchi.<br>vii. Kuendelea kufanya uchambuzi wa miradi inayoomba ufadhili wa mifuko ya mabadiliko ya tabianchi na idhini ya utekelezaji wa biashara ya Kaboni.<br>viii. Kutoa elimu kuhusu biashara ya kaboni kwa wadau wote, wakiwemo wafanya maamuzi, wananchi, wadau wa maendeleo, wanahabari na wawekezaji ili kuwa na uelewa wa pamoja kuhusu biashara ya Kaboni. |
| **2** | **MKATABA WA UMOJA WA MATAIFA WA KUPAMBANA NA KUENEA KWA HALI YA JANGWA (*UNITED NATIONS CONVENTION TO COMBAT DESERTIFICATION – UNCCD*).** | |
| 2.1 | Utangulizi | Tanzania ni nchi mwanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa kupambana na kuenea kwa hali ya Jangwa na Ukame (*United Nations Convention to Combat Desertification – UNCCD*). Mkataba huu ni kati ya Mikataba mitatu iliyopitishwa |

| | | |
|---|---|---|
| | | kwenye mkutano wa Mazingira na Maendeleo (*United Nations Conference on Environment and Development - UNCED*) uliofanyika nchini Brazil mwaka 1992. Tanzania ilijiunga na Mkataba huu mwaka 1992 na kuridhia mwezi Aprili, 1997.<br><br>Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais, inaratibu na kusimamia wa shughuli chini ya Mkataba huu ikiwa ni pamoja na Miradi inayolenga utekelezaji wa shughuli za Mkataba hasa Matumizi bora na endelevu ya ardhi (*Sustainable Land Management – SLM*), kushiriki mikutano ya nchi wanachama (*Conference of Parties – COPs*); Mikutano ya kupitia utekelezaji wa Mkataba (*Conference to review implementation of the Convention – CRIC*); Mikutano ya Kamati za Kisayansi za Mkataba (*Committee for Science and Technology – CST*) mafunzo mbalimbali. |
| 2.2 | Lengo la Mkataba | Malengo ya mkataba ni kama ifuatavyo:<br><br>(i) Mkataba wa UNCCD unalenga kuzijengea uwezo nchi zilizoathirika na kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame ili ziweze kupunguza madhara yatokanayo na hali hii.<br>(ii) Ili kufikia lengo hili, kifungu cha 9 (1) (Article 9 (1), kinazitaka nchi wanachama kuandaa Programu za Kitaifa za kupambana na kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame kwa njia shirikishi na kuanzia ngazi ya msingi (National Action Programmes to combat desertification - NAPs).<br>(iii) Lengo la NAP ni kuainisha visababishi vya kuenea kwa hali ya jangwa na kubuni njia muafaka za kupambana na visababishi hivyo na madhara yake hususan ukame.<br>(iv) Mipangokazi katika ngazi ya kanda ndogo na kanda zinaainisha changamoto mbalimbali zinazoweza kushughulikiwa kwa ushirikiano wa pamoja kati ya nchi za kanda ndogo |
| 2.3 | Hali ya uwasilishaji wa michango ya Nchi | Hadi kufikia mwaka 2019 kiasi cha Euro 7,136 kilikuwa kinadaiwa. Malipo haya yaliwasilishwa Wizara ya Mambo Nje na Ushirikiano wa Afrika mashariki ili wawasilishe deni hili Wizara ya Fedha kwa taratibu za malipo. |
| 2.4 | Shughuli zinazotekelezwa na Mkataba | Mkataba wa UNCCD unatekelezwa katika ngazi tatu (3) ambazo ni: -<br><br>• Ngazi ya taifa: Utekelezaji kupitia NAP; |

<table>
<tr><td></td><td></td><td>
<ul>
<li>Ngazi ya Kanda ndogo (Sub-region) Utekelezaji kupitia Sub-region Action Program (SRAP);</li>
<li>Ngazi ya Kanda (region): Region Action Program (RAP)</li>
</ul>
Utekelezaji wa Shughuli za Mkataba huu zilianza pale ambapo nchi yetu ilijiunga na Mkataba huu mwaka 1992, na ukomo wake ni pale ambapo nchi itaamua kujitoa katika Mkataba.
Kwa kuwa Tanzania ni mwanachama wa UNCCD shughuli zake zinatekelezwa nchi nzima na Wadau mbalimbali wenye uhusiano wa moja kwa moja na matumizi ya ardhi. Wadau hawa ni sekta za Kilimo, Misitu, Madini, Nishati, Maendeleo ya Makazi, Elimu, Viwanda, Washirika wa Maendeleo, Sekta Binafsi na Mashirika yasiyo ya Kiserikali.
</td></tr>
<tr><td>2.5</td><td>Changamoto</td><td>
<ul>
<li>Ushiriki hafifu wa Sekta katika masuala ya kupambana na kuenea kwa Jangwa;</li>
<li>Uelewa mdogo wa wananchi kuhusu masuala ya kupambana na kuenea kwa Jangwa;</li>
<li>Changamoto ya mafungu ya utekelezaji wa shughuli chini ya Mkataba; na</li>
<li>Changamoto ya uratibu wa shughuli chini ya Mkataba hasa Sekretarieti ya Mkataba.</li>
</ul>
</td></tr>
<tr><td>2.6</td><td>Hatua inayofuata</td><td>
<ol type="i">
<li>Kuratibu utekelezaji wa mpango jumuishi wa kurejesha ardhi iliyoharibika utokanao na kuenea kwa hali ya jangwa na ukame kwa kupunguza wa uzalishaji wa gesi joto na kuwezesha upatikanaji wa ajira kwa nchi za SADC (Great Green Wall Initiative);</li>
<li>Kukamilisha Mpango Kazi wa Kitaifa wa Kupambana na Kuenea kwa hali ya Jangwa na Ukame 2023 – 2027</li>
<li>Mkutano wa 16 wa nchi wanachama tarehe 2 – 13 Disemba, 2024 Jijini Riyadh Saudi Arabia;</li>
<li>Kutoa elimu kwa umma kuhusu kupunguza kuenea kwa hali ya jangwa na madhara yatokanayo na ukame;</li>
<li>Kikao cha Kamati ya kufanya mapitio utekelezaji wa Mkataba, 2023;</li>
<li>Kutoa elimu kwa umma kuhusu hatua zinazopaswa kuchukuliwa ili kupambana na kuenea kwa hali ya Jangwa;</li>
<li>Utekelezaji wa Programu ya Kuzifanya Nchi Wanachama kutokuwa na Uharibifu wa Ardhi kufikia mwaka 2030. (Land Degradation Neutrality Target Setting Program - LDN TSP)</li>
</ol>
</td></tr>
</table>

| | | |
|---|---|---|
| | | ambapo chini ya mradi wa Usimamizi Husishi wa Mazingira Katika Maeneo Kame ay Miombo Tanzania (Integrated Landscape Management In The Dry Miombo Woodland Of Tanzania) unaotekelezwa na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) katika Wilaya za Kaliua (Tabora) na Mlele (Katavi), OMR ina maeneo nane (Eight components) ya kutekeleza upande wa LDN; na<br>viii. Na kufuatilia fedha za kuendesha Ofisi ya Afisa Kiungo wa Mkataba. Fedha hizi zinatoka GEF kupitia UNEP Nairobi. Tayari UNEP Nairobi wamekwisha wasilisha Mkataba Mdogo wa Makubaliano (Small Scall Fund Agreement – SSFA) ambao umesainiwa na wao. Hivi sasa tunahitaji kibali kutoka Wizara yenye Dhamana ya Fedha ili OMR iweze kusaini kwa upande wetu. |
| **3** | **MKATABA WA RAMSAR WA USIMAMIZI WA MAENEO YA ARDHI OEVU (*RAMSAR CONVETION ON WETLANDS*)** | |
| 3.1 | Utangulizi | Tanzania ni mwanachama wa Mkataba wa Ramsar unaohusu matumizi endelevu ya ardhi oevu. Tanzania iliridhia mkataba huu tarehe 13 Agosti, 2000.<br><br>Katika kutekeleza Mkataba huu, Tanzania imesajili maeneo manne (RAMSAR Site) ambayo ni: Muyovozi katika mto Malagarasi-Kigoma, ardhi oevu ya bonde la Ziwa Natron-Manyara, bonde la mto Kilombero-Morogoro na bonde la Rufiji-Mafia hadi Kilwa-Pwani. |
| 3.2 | Lengo la Mkataba | Kuhifadhi na kuzuia upotevu wa maeneo yenye ardhi oevu duniani kote, kupitia matumizi endelevu ya rasilimali zinazopatikana katika maeneo hayo. |
| 3.3 | Hali ya uwasilishaji wa Michango ya Nchi | Tanzania inachangia kiasi cha Faranga za Uswis (*Swis franc*) CHF1,000 kwa mwaka. Hadi sasa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inadaiwa jumla ya kiasi cha CHF 13,000 ikiwa ni deni la malimbikizo ya mchango kwa kipindi cha kuanzia 2011 hadi 2023 ambalo limewasilishwa Hazina. |
| 3.4 | Shughuli zinazotekelezwa na Mkataba | i) Kuandaa Mwongozo wa Usimamizi wa Maeneo ya ardhi oevu wa mwaka 2014, ili kuziwezesha Wizara, taasisi na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuweza kusimamia kwa ufanisi maeneo yaliyo chini ya himaya zao;<br>ii) Mapitio ya Mkakati wa Kuhifadhi Mazingira ya Bahari, |

| | | |
|---|---|---|
| | | Ukanda wa Pwani, Maziwa, Mito na Mabwawa wa mwaka 2008 na kuwa na Mkakati mpya wa Kuhifadhi Mazingira ya Bahari, Ukanda wa Pwani, Maziwa, Mito na Mabwawa 2021-2026;<br>iii) Mapitio ya Mkakati wa Kuhifadhi Mazingira ya Ardhi na vyanzo vya Maji wa mwaka 2006 na kuwa na Mkakati wa Kuhifadhi Mazingira ya Ardhi na Vyanzo vya Maji 2021 – 2026;<br>iv) Kufanya tathmini ya hali ilivyo ya maeneo ya ardhi oevu nchini |
| 3.5 | Mafanikio | i) Kupata ufadhili wa miradi midogo inayohusu usimamizi wa maeneo ya Ramsar<br>ii) Utekelezaji wa mradi wa hifadhi ya ardhi oevu katika eneo la Ramsar la Bonde la Kilombero ambapo elimu ya hifadhi na matumizi endelevu imetolewa katika eneo.<br>iii) Kupata usaidizi wa kitaalam kutoka Sekretarieti kuhusu usimamizi endelevu wa Maeneo ya ardhi oevu yakiwemo maeneo ya Ramsar.<br>iv) Kubadilishana uzoefu miongoni mwa nchi wanachama wa mkataba katika usimamizi wa maeneo ya ardhi oevu na Ramsar.<br>v) Kuimarisha ushirikiano na jumuiya ya kimataifa katika usimamizi wa maeneo ya ardhi oevu. |
| 3.6 | Changamoto | i) Uelewa mdogo wa jamii kuhusu hifadhi na usimamizi wa maeneo oevu<br>ii) Uvamizi wa maeneo ya ardhi oevu kwa ajili ya shughuli zisizo endelevu za kibinadamu zikiwemo, kilimo, kuosha magari, kufyatua matofali<br>iii) Usimamizi hafifu kwa mamlaka zinazohusika na usimamizi wa maeneo ya ardhi oevu |
| 3.7 | Ushiriki wa Mikutano | Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hushiriki katika mikutano chini ya Mkataba huu. Mikutano ya mkataba huu hufanyika kila mwaka katika ngazi za kimataifa na kikanda. Mkutano Mkuu (COP) hufanyika kila baada ya miaka mitatu (3), Mikutano ya kitaalamu Standing Committee – SC) na Mikutano ya Kikanda hufanyika kila mwaka RAMCEA.<br>Manufaa ya kushiriki katika mikutano hii ni pamoja na:<br>i. Kuimarisha ushirikiano na jumuiya ya kimataifa na kikanda |

| | | |
|---|---|---|
| | | katika kusimamia maeneo ya ardhi oevu hususan matumizi ya teknolojia mpya na za kisasa.<br>ii. Upatikanaji wa fedha za kutekeleza miradi kutoka Sekretarieti na wadau wengine wa maendeleo<br>iii. Kuhakikisha msimamao na maslahi ya nchi yanawasilishwa kwenye mkutano na yanajumuiswa katika maazimio ya mkutano na mipango ya Mkataba<br>iv. Kuongeza ujuzi na kubadilishana uzoefu wa mbinu mbalimbali na bora ya kushughulikia changamoto za uharibifu wa maeneo ya ardhi oevu |
| 3.8 | Hatua inayofuata | i. Kuandaa maandiko ya miradi na kutafuta fedha za kutekeleza miradi inayolenga kuhifadhi ardhi oevu katika mabonde ya Mto Ruaha Mkuu, Kilombero, Mto Mara, Malagarasi na mifumo-ikolojia ya maeneo kame;<br>ii. Kuandaa taarifa za utekelezaji wa Mkataba na kuwasilisha sekretarieti.<br>iii. Kuandaa Ripoti ya Taifa ya utekelezaji wa Mkataba ambayo itawasilishwa katika Mkutano wa 15 wa Nchi wanachama utakao fanyika mwaka 2025, Victoria Falls, Zimbabwe.<br>iv. Kuandaa kanuni ya Maeneo lindwa na Maeneo Nyeti kwa Mazingira yakiwemo maeneo ya Ardhioevu;<br>v. Kutoa elimu kwa umma kuhusu hifadhi ya ardhi oevu. |
| *4* | **MKATABA WA KIMATAIFA WA HIFADHI YA BIOANUAI *(UNITED NATIONS CONVENTION ON BIOLOGICAL DIVERSITY-CBD)*** | |
| 4.1 | Utangulizi | Mkataba wa Kimataifa wa Hifadhi ya Bioanuai unaohusu hifadhi na matumizi endelevu ya bioanuai. Tanzania iliridhia mkataba huu mwaka 1996. Aidha, Mkataba huu unatekelezwa kupitia Itifaki tatu ambazo ni; -<br><br>Itifaki ya Catargena inayohusu Usimamizi wa Matumizi Salama ya Bioteknolojia ya Kisasa ambayo imeridhiwa tarehe 16 March 2003;<br><br>Itifaki ya Nagoya Kuhusu Upatikanaji na Mgawanyo Sahihi wa Rasilimali za Kijenetiki zitokanazo na Bioanuai, ambayo imeridhiwa tarehe 19 Aprili, 2018*;* na<br><br>Itifaki ya ziada ya Nagoya Kuhusu Uwajibikaji Kisheria na Fidia kwa madhara yatokanayo na Bioteknolojia ya Kisasa ambayo iliridhiwa tarehe 16 Septemba, 2019. |

| | | |
|---|---|---|
| 4.2 | Lengo la Mkataba | Mkataba unazitaka nchi wanachama kuchukua hatua za kuhifadhi na matumizi endelevu ya bioanuai pamoja na upatikanaji na mgawanyo sahihi wa rasilimali za kijenetiki zitokanazo na bioanuai. |
| 4.3 | Shughuli zinazotekelezwa na Mkataba | i. Kuandaliwa na kupitiwa kwa Sera, Sheria, Mikakati na Miongozo ya Sekta mbalimbali ikiwemo: kilimo, madini, Mifugo, uvuvi, umwagiliaji, maji, afya, wanyamapori na elimu ili kuhuishwa masuala ya Hifadhi ya Bioanuai kwenye bajeti na mipango kazi ya sekta hizo;<br>ii. Uandaaji na utekelezaji wa Mkakati na Mpango Kazi wa Taifa wa Hifadhi ya Bioanuai;<br>iii. Kuanzishwa kwa Kampeni ya Upandaji Miti ambapo kila Wilaya inatakiwa kupanda na kutunza miti isiyopungua milioni 1.5 kwa mwaka;<br>iv. Kuandaliwa na kutekelezwa kwa miradi na Program mbalimbali za hifadhi ya bioanuai;<br>v. Uhamasishaji na kujengewa uelewa kwa jamii kuhusu usimamizi na hifadhi ya bioanuai. |
| 4.4 | Mafanikio | i. Tanzania tumeweza kupata fedha nyingi za kigeni kutoka mifuko ya kimataifa na wadau wa maendeleo kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya hifadhi ya bioanuai hapa nchini.<br>ii. Jamii kuweza kufaidika na utekelezaji wa miradi ya hifadhi bioanuai kwa kuwa miradi mingi Pamoja na mambo mengine inalenga kuongeza kipato kwa jamii.<br>iii. Kuimarika kwa ushirikiano na jumuiya za kimataifa katika nyanja za utafiti na uendelezaji wa teknolojia za hifadhi ya bioanuai.<br>iv. Jamii imejengewa uelewa kuhusu hifadhi ya bioanuai<br>i. Upatikanaji wa fursa za mafunzo kwa wanafunzi wa ngazi mbalimbali kuhusu hifadhi ya bioanuai |
| 4.5 | Changamoto | ii. Uelewa mdogo wa jamii kuhusu hifadhi na usimamizi wa bioanuai<br>i. Uvamizi wa maeneo ya hifadhi na maeneo tengefu kwa ajili ya shughuli za kibinadamu zisizo endelevu zikiwemo, kilimo, kufyatua matofali, ukataji miti holela kwa kuni na |

| | | |
|---|---|---|
| | | mkaa, mifugo mingi inayozidi kiwango cha malisho. |
| 4.6 | Ushiriki kwenye Mikutano | Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hushiriki katika mikutano chini ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa ambayo hufanyika kila mwaka katika ngazi za kimataifa na kikanda. Mkutano Mkuu (COP) hufanyika kila ya baada ya miaka miwili, Mikutano ya kitaalamu SBST, SBI hufanyika kila mwaka. Aidha, kwa mwaka 2023 Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haijashiriki kwenye mkutano.<br><br>Matarajio ya kushiriki mikutano:<br><br>v. Upatikanaji wa fedha za kutekeleza miradi kutoka mifuko ya kimataifa na wadau wa maendeleo<br>vi. Kuimarisha ushirikiano na jumuiya ya kimataifa katika nyanja za utafiti na uendelezaji wa teknolojia za Hiadhi ya Bioanuai<br>vii. Kuendeleza majadaliano na taasisi za kimataifa kuhusu ufadhili wa miradi ya hifadhi ya bioanuai<br>viii. Kupata ujuzi na kubadilishana uzoefu wa mbinu mbalimbali na bora ya kushughulikia changamoto za upotevu wa bioanuai<br>ix. Kupanua wigo wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya miradi ya hifadhi ya bioanuai.<br>iii. Kuhakikisha kuwa msimamao na maslahi ya nchi yanawasilishwa kwenye mkutano na yanajumuiswa katika maazimiao ya mkutano |
| 4.7 | Hatua inayofuata | i. Kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu hifadhi ya bioanuai na matumizi salama ya baioteknolojia ya kisasa<br>ii. Kuandaa maandiko ya miradi kuhusu hifadhi ya bioanuai<br>iii. Kuandaa kanuni na mwongozo wa mgawanyo wa faida zinatokana na matumizi ya jeni kibaiolojia.<br>iv. Kuratibu maandalizi ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kushiriki katika mkutano wa 26 wa nchi wanachama wa Hifadhi ya bioanuai utakaofanyika Uturuki mwaka 2024.<br>v. Kuandaa na kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa Mkataba wa hifadhi ya bioanuai sekretarieti ya Mkataba.<br>vi. Mkutano wa Kamati ya Usimamizi wa Utekelezaji wa |

| | | |
|---|---|---|
| | | Mkataba Machi, 2023, Ujerumani.<br>iv. Kuandaa Mkakati na Mpango Kazi wa Taifa wa Hifadhi ya Bioanuai (NBSAP) 2023-2028. |
| **5** | **MKATABA WA USIMAMIZI ENDELEVU WA ZIWA TANGANYIKA (THE CONVENTION ON THE SUSTAINABLE MANAGEMENT OF LAKE TANGANYIKA)** | |
| 5.1 | Utangulizi | Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni nchi mojawapo kati ya nchi nne (4) mwanachama wa Mkataba wa Kikanda wa usimamizi endelevu wa Ziwa Tanganyika. Nchi zingine ni Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), Burundi na Zambia. Tanzania iliridhia Mkataba huu mwaka 2004. |
| 5.2 | Lengo la Mkataba | Usimamizi endelevu wa hifadhi ya mazingira ya Ziwa Tanganyika miongoni mwa nchi zinazounganishwa wa Ziwa Tanganyika. |
| 5.3 | Hali ya uwasilishaji wa Michango ya Nchi | Tanzania inawajibu wa kuchangia kiasi cha fedha za kimarekani 303,900. Kwa sasa hakuna deni |
| 5.4 | Shughuli zinazotekelezwa na Mkataba | i. Kushiriki katika Mkutano wa 12 wa Kamati ya wataalamu wa nchi wanachama Zambia Novemba, 2023;<br>ii. Kushiriki katika Mkutano wa 11 wa Mawaziri wa usimamizi endelevu wa Ziwa Tanganyika nchini Zambia Novemba, 2023;<br>iii. Kutathmini utekelezaji wa miradi ya hifadhi na usimamizi endelevu wa Ziwa Tanganyika (PRODAPI) katika mikoa ya Kigoma, Katavi na Sumbawanga;<br>iv. Kuandaa vipaumbele vya Programu endelevu ya Maendeleo ya Kanda ya Ziwa Tanganyika awamu ya pili (PRODAP II);<br>v. Ziara za kutathmini utekelezaji wa miradi, (LATAWAMA na LATAFIMA katika mkoa wa Kigoma;<br>vi. Kufanya tathmini ya maeneo muhimu ambayo yanafaa kwa ajili ya ufugaji wa Samaki kwa njia ya Vizimba;<br>vii. Kutoa elimu kwa jamii ya wavuvi inayozunguka Ziwa Tanganyika kuhusu uvuvi endelevu, hususan usitishaji wa shughuli za uvuvi katika kipindi cha kuanzia tarehe 15 Mei hadi 15 Agosti ya kila mwaka kwa kipindi cha miaka mitatu;<br>viii. Kuendesha warsha za kukuza na kujenga uelewa kuhusu Utekelezaji wa Mkataba wa Kikanda wa Nchi wanachama wa Mamlaka ya Ziwa Tanganyika. |

| | | |
|---|---|---|
| 5.5 | Mafanikio | i. Nchi wanachama kufaidika na utekelezaji wa miradi ya hifadhi ya rasilimali za Ziwa Tanganyika kwa kuwa miradi mbalimbali ambayo inanufaisha jamii inayozunguka Ziwa Tanganyika.<br>ii. Kuimarika kwa ushirikiano miongoni mwa nchi wanachama katika kufanya utafiti na uendelezaji wa teknolojia za kusimamia na kuhifadhi Ziwa Tanganyika.<br>ii. Jamii inayozunguka Ziwa kujengewa uelewa kuhusu hifadhi ya Ziwa Tanganyika<br>v. Kusainiwa kwa Itifaki ya kuanza ufugaji wa Samaki kwa Njia ya Vizimba katika Ziwa Tanganyika ambayo itakuwa suluisho la upungufu wa Samaki katika Ziwa hilo<br>v. Kukubalika kuwepo kwa nafasi ya Makatibu Wakuu katika muundo wa Mamlaka ya Usimamizi wa Ziwa Tanganyika ambapo awali nafasi hiyo haikuwepo. |
| 5.6 | Changamoto | i) Uelewa mdogo wa jamii inayozunguka maeneo ya Ziwa kuhusu hifadhi na usimamizi wa rasilimali zinazopatikana katika Ziwa Tanganyika;<br>ii) Usimamizi hafifu wa mamlaka zinazohusika na usimamizi wa maliaisli zinazopatikana katika Ziwa Tanganyika |
| 5.7 | Ushiriki kwenye Mikutano | Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hushiriki katika mikutano chini ya Mkataba huu. Mikutano ya mkataba huu hufanyika kila mwaka katika ngazi za kimataifa na kikanda. Mkutano Mkuu ni Mkutano wa Mawaziri(Conference of Ministers - CoM) hufanyika kila mwaka. Aidha, Mikutano ya kitaalamu Management Committes – MC) na Mikutano ya Kamati ndogo ndogo hufanyika kila mwaka mara mbili (2).<br><br>Manufaa ya kushiriki katika mikutano hii ni pamoja na:<br>i) Kuimarisha ushirikiano na jumuiya ya kikanda katika kusimamia Ziwa Tanganyika;<br>ii) Upatikanaji wa fedha za kutekeleza miradi kutoka kwa Wafadhili, Sekretarieti na wadau wengine wa maendeleo;<br>iii) Kuhakikisha msimamo na maslahi ya nchi yanawasilishwa kwenye mkutano yanajumuiswa katika maazimio ya mkutano na mipango ya Mkataba huu;<br>iv) kubadilishana uzoefu wa mbinu mbalimbali na bora ya |

| | | |
|---|---|---|
| | | kushughulikia changamoto za usimamizi wa Ziwa Tanganyika. |
| 5.8 | Hatua inayofuata | i) kukamilisha uanzishwaji wa Programu endelevu ya Maendeleo ya Kanda ya Ziwa Tanganyika (PRODAP II);<br>ii) Kuandaa mradi wa usimamizi endelevu wa maji na usimamizi wa taka katika Ziwa tanganyika awamu ya Pili (LATAWAMA -II)<br>iii) Kushiriki katika maandalizi ya Mkutano wa 13 wa Kamati ya wataalamu wa nchi wanachama Jamhuri ya Kongo Agosti, 2024;<br>iv) Kukamilisha uanzishaji wa mradi wa hifadhi wa Bioanuai katika Ziwa Tanganyika utakaofadhiliwa na UNEP/GEF, mradi ambao unatarajiwa kuanza hivi karibuni;<br>v) Kutoa elimu kwa jamii ya wavuvi wa Mwambao mwa Ziwa Tanganyika kuhusu utekelezaji wa Mkataba wa Usimamizi ensdelevu wa rasilimali za Ziwa ambapo Ziwa Tanganyika litapumzishwa shughuli za uvuvi kwa kipindi cha miezi mitatu kuanzia tarehe 15 Mei hadi 15 Agosti ya kila mwaka kwa miaka mitatu. |
| **6** | **MKATABA WA VIENNA UNAOHUSU HIFADHI YA TABAKA LA OZONI NA ITIFAKI YA MONTREAL KUHUSU KEMIKALI ZINAZOMONG’ONYOA TABAKA LA OZONI** | |
| 6.1 | Utangulizi | Mkataba wa Vienna unaohusu hifadhi ya Tabaka la Ozoni ulisainiwa na nchi wanachama mwaka 1985.<br><br>Mkataba huu ulilenga kuweka ushirikiano miongoni mwa nchi wanachama katika kupeana taarifa za tafiti kuhusu maendeleo ya tabaka la Ozoni lililokuwa limeanza kumo’ngonyoka. Mkataba wa Vienna haukuwa na mamlaka ya kisheria ya kudhibiti uharibifu wa tabaka hususan udhibiti wa kemikali zinazoharibu tabaka la ozoni.<br><br>Ili kuweka mamlaka ya kisheria, mnamo mwaka 1987 nchi wanachama wa Mkataba wa Vienna zilitia saini Mkataba mdogo (Itifaki) ya Montreal inayohusu udhibiti wa kemikali zinazomong’onyoa tabaka la ozoni, ambapo Tanzania iliridhia mwaka 1993. |
| 6.2 | Lengo la Mkataba na Itifaki | Lengo la Mkataba wa Vienna ni kulinda Tabaka la Ozoni na kulinda afya ya binadamu na mazingira dhidi ya madhara |

| | | |
|---|---|---|
| | | yanayotokana na kuharibiwa kwa tabaka la Ozoni.<br><br>Lengo la Itifaki ya Montreal ni kudhibiti kemikali zinazomongónyoa tabaka la Ozoni kulinda afya ya binadamu na mazingira dhidi ya madhara yanayotokana na kuharibiwa kwa tabaka la Ozoni. |
| 6.3 | Hali ya uwasilishaji wa michango ya Nchi | Tanzania kama nchi inayoendelea haichangii katika itifaki hii. Shughuli za Itifaki ya Montreal zinaendeshwa kwa bajeti ya fedha zinazofadhiliwa na Mfuko wa Utekelezaji wa Itifaki ya Montreal (*Multilateral Fund (MLF) for Implementation of Montreal Protocol.* |
| 6.4 | Shughuli zinazotekelezwa na Mkataba | Utekelezaji wa Itifaki ya Montreal umekuwa ukifanyika kupitia utekelezaji shughuli mbalimbali kama ifuatavyo:<br><br>• Utekelezaji wa Mpango wa kuondosha kemikali jamii ya Hydrochlorofluorocarbons (HCFCs) ifikapo mwaka 2030 ikiwemo kujenga uwezo wa mafundi mchundo, kujenga uwezo kwa Taasisi za udhibiti mipakani (Hydrochlorofluorocarbons (HCFC) Phase-out Management Plan–HPMP, 2023-2025);<br>• Utekelezaji wa shughuli wezeshi ya kujenga uwezo wa Kitaasisi katika kutekeleza Itifaki ya Montreal (Institutional Strengthening Project for the Implementation of Montreal Protocol), ikiwemo ukusanyaji na uwasilishaji wa takwimu za uingizaji wa kemikali nchini, elimu kwa waingizaji wa kemikali nchini na kujenga uwezo wa Taasisi katika kusimamia matakwa ya Itifaki.<br>• Utekelezaji wa shughuli wezeshi ya kuiwezesha Tanzania kuridhia Marekebisho ya Kigali ya kupunguza uzalishaji na matumizi ya kemikali jamii ya Hydrofluorocarbons (HFCs) chini ya Itifaki ya Montreal ikiwemo kuweka mifumo ya kisheria ya kudhibiti uingizaj na matumizi ya kemikali husika *(Enabling Activities for Early ratification of Kigali Amendment to the Montreal Protocol on Phasing Down Hydrofluorocarbons).* |
| 6.5 | **Mafanikio** | (i) Upatikanaji wa fedha za kutekeleza miradi kutoka mifuko ya kimataifa na wadau wa maendeleo<br><br>(ii) Kuimarisha ushirikiano na jumuiya ya kimataifa katika nyanja za utafiti na uendelezaji wa teknolojia za hifadhi |

| | | |
|---|---|---|
| | | ya tabaka la ozoni na mabadiliko ya tabianchi.<br>(iii) Kuongeza upatikanaji wa fedha za kigeni kutokana na fedha za miradi zinazoletwa nchini<br>(iv) Kuongeza uelewa kwa jamii kuhusu hifadhi ya tabaka la ozoni, mabadiliko ya tabianchi na athari zake<br><br>Upatikanaji wa fursa za mafunzo kwa wanafunzi wa ngazi mbalimbali pamoja na wakufunzi kuhusu hifadhi ya tabaka la ozoni na mbadiliko ya tabianchi |
| 6.6 | **Changamoto** | i. Gharama kubwa za teknolojia na vifaa vya kutambua kemikali/gesi zinazoharibu tabaka la ozoni na kuchangia ongezeko la joto duniani.<br>ii. Uelewa mdogo wa jamii kuhusu umuhimu wa kuhifadhi tabaka la ozoni.<br>iii. Uhaba wa vifaa vya kutambua kemikali/gesi zinazoharibu tabaka la ozoni pamoja na mitambo ya kusafisha gesi. |
| 6.7 | Hatua inayofuata | i. Kutekeleza awamu ya pili ya Mpango wa kuondosha kemikali jamii ya *Hydrochlorofluorocarbons (HCFCs) (Hydrochlorofluorocarbons (HCFC) Phase-out Management Plan–HPMP, 2023- 2028, Stage II*;<br>ii. Kutekeleza Awamu ya nane ya shughuli wezeshi ya kujenga uwezo wa Kitaasisi katika kutekeleza Itifaki ya Montreal (*Institutional Strengthening Project for the Implementation of Montreal Protocol - Phase VII, 2023-2025*).<br>iii. Kuandaa Mpango wa Kitaifa wa Kutekeleza Marekebisho ya Kigali ya kupunguza uzalishaji na matumizi ya kemikali jamii ya *Hydrofluorocarbon* chini ya Itifaki ya Montreal (Preparation of a Kigali HFC implementation Plan)<br>iv. Kuandaa na kuwasilisha taarifa ya utekelezaji ya Mkataba |
| **7** | **MKATABA WA MINAMATA KUHUSU USIMAMIZI WA ZEBAKI** | |
| 7.1 | Utangulizi | Mkataba wa Minamata ni makubaliano ya kimataifa kuhusu udhibiti na usimamizi wa uchafuzi wa mazingira utokanao na kemikali aina ya Zebaki unaochangiwa na shughuli za binadamu kama vile uchimbaji wa madini na shughuli za viwandani. Mkataba huu ulianzishwa mwaka 2013 na mpaka sasa umeridhiwa na nchi wanachama 143.<br><br>Tanzania iliridhia Mkataba huu mwaka 2020. |

| | | |
|---|---|---|
| 7.2 | Lengo la Mkataba | Lengo Mkataba ni kulinda afya ya binadamu na mazingira dhidi ya madhara ya Zebaki na bidhaa zake. |
| 7.3 | Hali ya uwasilishaji wa michango ya Nchi | Tanzania huchangia takribani kiasi cha Dola za Marekani 365 kwa mwaka. Aidha, kuanzia mwaka 2018 – 2022 Tanzania imechangia ada ya uanachama wa Mkataba kiasi cha Dola za Marekani 729. |
| 7.4 | Shughuli zinazotekelezwa na Mkataba | i. Kuandaa taarifa za utekezaji wa Mkataba na kuwasilisha Sekretarieti ya Mkataba kila baada ya miaka miwili;<br>ii. Kutoa elimu kwa umma kuhusu maudhui ya Mkataba na madhara ya Zebaki kwa wadau mbalimbali;<br>iii. Kuratibu ushiriki wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika mkutano wa Kikanda na Nchi wanachama wa Mkataba wa Minamata; na<br>iv. Kuandaa maandiko mbalimbali ya miradi kuwezesha utekelezaji wa Mkataba husika; na<br>v. Kutekeleza miradi mbalimbali na shughuli wezeshi zinazotekelezwa chini ya Mkataba. |
| 7.5 | Mafanikio | i. Kusaidia kulinda afya ya binadamu na mazingira dhidi ya madhara ya zebaki;<br>ii. Upatikanaji wa fedha kwa ajili ya miradi; na<br>iii. Kuongezeka kwa uelewa kuhusu madhara yatokanayo na zebaki |
| 7.6 | Ushiriki wa mikutano | Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hushiriki katika mikutano chini ya Mkataba wa Minamata ambayo hufanyika kila baada ya mwaka mmoja katika ngazi za kimataifa na kikanda. Mikutano ambayo Jamhuri ya Muungano imeshiriki kwa mwaka 2023 ni:<br>• Mkutano wa kikanda uliofanyika Geneva Uswisi; na<br>• Mkutano wa nchi wanachama wa Mkataba uliofanyika Geneva Uswisi.<br>Fursa na Matarajio<br>• Upatikanaji wa fedha za *Special Programme* kutekeleza shughuli zinazoratibiwa chini ya Mkataba husika; na |

| | | |
|---|---|---|
| | | Kuendelea kushirikiana na nchi mabalimbali katika kupambana na usafirishaji na uuzaji haramu wa zebaki. |
| 7.7 | Changamoto | i. Kuchelewa kwa taarifa za utekelezaji wa Mkataba kutoka taasisi nyingine zinazotekeleza shughuli za mkataba huu;<br>ii. Usafirishaji na uuzaji haramu wa zebaki;<br>iii. Baadhi ya wachimbaji wadogo wa dhahabu kutokutumia vifaa kinga katika shughuli za uchenjuaji;<br>iv. Kuchelewa kwa taarifa za utekelezaji wa Mkataba kutoka taasisi nyingine zinazotekeleza shughuli za mkataba huu;<br>v. Usafirishaji na uuzaji haramu wa zebaki;<br>vi. Baadhi ya wachimbaji wadogo wa dhahabu kutokutumia vifaa kinga katika shughuli za uchenjuaji. |
| 7.8 | Hatua inayofuata | i. Kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu maudhui ya Mkataba na madhara ya Zebaki;<br>ii. Kuendelea kuratibu ushiriki wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika mikutano ya Kikanda na Nchi wanachama wa Mkataba wa Minamata;<br>iii. Kuandaa taarifa ya utekelezaji wa Mkataba; na<br>iv. Kuandaa maandiko ya miradi kuwezesha utekelezaji wa Mkataba husika pale fursa zinapopatikana. |
| **8** | **MKATABA WA BASEL KUHUSU UDHIBITI WA USAFIRISHAJI WA TAKA HATARISHI BAINA YA NCHI NA NCHI NA UTUPAJI WAKE.** | |
| 8.1 | Utangulizi | Mkataba wa Basel unahusu udhibiti wa usafirishaji wa taka hatarishi baina ya nchi na nchi na utupaji wake. Mkataba huu ulianzishwa mwaka 1989 na ulianza kutekelezwa rasmi mwaka 1992. Tanzania iliridhia Mkataba huu mwaka 1993.<br><br>Hadi sasa kufikia Mei, 2023, Mkataba una jumla ya nchi wanachama 191.<br><br>Jumla ya aina 47 za taka hatarishi zinadhibitiwa na Mkataba wa Basel. Taka hatarishi ni pamoja na vyuma chakavu; betri chakavu; taka za plastiki; mafuta chakavu; mipira chakavu; mafuta machafu; taka za kielektroniki na taka zote zitokanazo na shughuli za migodi. |

| | | |
|---|---|---|
| | | Mkataba wa Basel umeweka mfumo wa upashanaji habari na kupata ridhaa kutoka Mamlaka za usimamizi wa Mkataba wa Basel ya nchi zinazotegemea kupokea taka kabla ya kusafirishwa kwenda nchi hiyo (*Prior Informed Consent*). |
| 8.2 | Lengo la Mkataba | Lengo la Mkataba ni pamoja na: -<br><br>-Kupunguza uzalishaji wa taka hatarishi ili kulinda afya ya binadamu na mazingira;<br><br>-Kudhibiti usafirishaji wa taka hatarishi baina ya nchi na nchi;<br><br>-Kukuza ushirikiano wa pamoja baina ya nchi wanachama katika udhibiti wa taka hatarishi;<br><br>-Kuepuka baadhi ya nchi kufanya nchi zingine dampo la taka hatarishi wanazozalisha; na<br><br>Kuweka mifumo halali ya shughuli za taka hatarishi kwenye nchi husika ikiwa ni pamoja na ukusanyaji, uhifadhi na usafirishaji. |
| 8.3 | Hali ya uwasilishaji wa michango ya Nchi | Hadi kufikia Januari, 2024 Tanzania inadaiwa mchango wa mwaka mmoja kiasi cha dola za Kimarekani 512 baada ya kulipia michango ya miaka mitatu mfululizo kuanzia mwaka 2021 hadi 2023 kiasi cha Dola za Kimarekani 1,467 mnamo Januari, 2023. Aidha, Ofisi inatarajia kuiandikia Wizara ya Fedha kwa ajili ya kuwasilisha mchango kwa ajili ya malipo ya kiasi cha dola za Kimarekani 512 ikiwa ni mchongo wa mwaka 2024 kulingana na hati ya madai iliyowasilishwa na Sekretarieti ya Mkataba husika Januari 2024. |
| 8.4 | Shughuli zinazotekelezwa na Mkataba | i) Kutekeleza shughuli wezeshi chini ya Mkataba ambapo kwa sasa Tanzania inatekeleza Mradi ifuatayo: -<br><br>Kuandaa Mkakati wa Kikanda wa Usimamizi wa Taka za Plastiki zinazovuka mipaka. Chini ya shughuli hii wezeshi shughuli zifuatazo zimefanyika: -<br><br>• Inception workshop ya kuunda Kikosi kazi cha Taifa kwa ajili ya kushirikiana na OMR kuratibu utekelezaji wa Mradi; |

| | | |
|---|---|---|
| | | • Kufanya Tathmini ya uwezo wa Kitaasisi katika kusimamia taka za plastiki zinazovuka mipaka; na<br>• Kufanya tathmini ya uingizaji na matumizi ya bidhaa za plastiki kunakochangia uzalishaji wa taka nchini.<br><br>Mradi wa Majaribio ya Usimamizi na Udhibiti wa uingizaji nchini wa Taka za Kielektroniki na vifaa vya Umeme (***Pilot Project on electric and electronic equipment (UEEE) by using Basel Convention E-waste Technical Guideline (Reduce Waste Project).***<br>ii) Kusimamia utekelezaji wa Kanuni za Usimamizi na Udhibiti wa Taka Hatarishi za Mwaka 2021 na Kanuni za Usimamizi na Udhibiti wa Taka za Kielektroniki za Mwaka 2021 kwa kumshauri Waziri mwenye Dhamana kutoa vibali; |
| 8.5 | Mafanikio | i) Upatikanaji wa rasilimali fedha kupitia Miradi inayotekelezwa nchini;<br>ii) Misaada ya kitaalamu;<br>iii) Kuongezeka wa uelewa wa jamii kuhusu taka hatarishi na madhara yake kwa afya ya binadamu na mazingira; na<br>iv) Ushiriki wa nchi kwenye warsha za Kikanda za kuongeza uelewa, kuainisha changamoto, na kujadili masuala muhimu ikiwemo kuainisha vipaumbele kuhusu udhibiti na usimamizi wa taka hatarishi |
| 8.6 | Ushiriki wa Mikutano | i) Kushiriki kwenye vikao vya Kikanda ambapo nchi wanachama hupata nafasi ya kukutana, kujadili masuala muhimu ya Mkataba, kuainisha vipaumbele na changamoto za kikanda kwa ajili ya kuziwasilisha kwenye vikao vya nchi wanachama;<br>ii) Kushiriki kwenye Mikutano ya nchi wanachama wa Mkataba wa Basel; ambapo nchi hupata nafasi ya kuchangia Msimamo wa masuala ya usimamizi wa Taka hatarishi kulingana na Agenda zinazobainishwa. Mkutano wa mwisho Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kushiriki ulifanyika mwezi Mei, 2023 ambapo pamoja na masula mengine nchi wanachama zilifanya majadiliano na kukubaliana kuhusu kuongeza kasi na kuboresha utekelezaji wa Mkataba wa Basel katika kufikia malengo yenye tija juu ya usimamizi wa |

| | | |
|---|---|---|
| | | taka za plastiki; taka za kielektroniki; taka za betri chakavu; taka za mipira chakavu na taka zitokanazo na kemikali zimazodumu kwenye mazingira kwa muda mrefu.<br>iii) Kushiriki Warsha kuhusu usimamizi na udhibiti wa taka hatarishi zinazoratibiwa na Sekretarieti ya Mkataba, vituo vya Kikanda na wadau wengine. |
| 8.7 | Changamoto | i. Baadhi ya nchi kuchelewa ama kutokutoa kabisa Idhini ya kupokea taka zinazosafirishwa nje ya nchi;<br>xiv. Baadhi ya nchi kuingiza taka nchini bila kufuata taratibu na matakwa ya nchi;<br>xv. Baadhi ya wafanyabiashara nchini kufanya shughuli za taka hatarishi bila ya kuwa na vibali vilivyotolewa na Waziri; na<br>xvi. Baadhi ya wadau wasiokuwa waaminifu kuhujumu miundombinu ya nchi kwa ajili ya biashara ya vyuma chakavu. |
| 8.8 | Hatua inayofuata | i) Kukamilisha uandaaji wa Mfumo wa kielektroniki wa maombi ya vibali vya Taka hatarishi kwa kuushirikiana na NEMC;<br>ii) Kushiriki kukamilisha Mkakati wa kikanda wa usimamizi wa taka za plastiki zinazovuka mipaka;<br>iii) Kukamilisha rasimu ya Mwongozo wa Taifa wa Udhibiti na Usimamizi wa Taka hatarishi;<br>iv) Kushiriki vikao vya nchi; Kikanda; na Kimataifa vya kuboresha Usimamizi wa Taka Hatarishi; na<br>v) Kufiatilia upatikanaji wa rasilimali fedha kwa ajili ya kupata Miradi ya Usimamizi wa Taka Hatarishi. |
| **9** | **MKATABA WA STOCKHOLM KUHUSU UDHIBITI WA KEMIKALI ZINAZODUMU KWENYE MAZINGIRA KWA MUDA MREFU** | |
| 9.1 | **Utangulizi** | Tanzania ni Nchi mwanachama wa Mkataba wa Stockholm kuhusu Udhibiti wa Kemikali zinazodumu kwenye Mazingira kwa Muda Mrefu (Stockholm Convention on Persistent Organic Pollutants- POPs). Idadi ya kemikali zinazodhibitiwa chini ya Mkataba huu ni 28 ambazo ni kemikali za viwandani, Viuatilifu na kemikali zinazozalishwa bila kutarajia kutokana na shughuli za binadamu. |

| | | |
|---|---|---|
| 9.2 | **Lengo la Mkataba** | Kulinda afya ya binadamu na mazingira kutokana na athari za kemikali zinazodumu kwenye mazingira kwa muda mrefu |
| 9.3 | **Hali ya uwasilishaji wa michango ya Nchi** | Nchi wanachama wa Mkataba zinapaswa kuwasilisha michango yao kwenye Sekretarieti kila mwaka. Aidha, Tanzania imechangia mara ya mwisho mwaka 2022 ambapo ilichangia fedha kiasi cha Dola za Marekani 242 kati ya 677 zilizopaswa kuchangiwa. Kwa mwaka 2023, tulipaswa kuchangia Dola za Marekani 331. Had sasa, deni la mchango ni Dola za Marekani 766 ambalo limewasilishwa HAZINA kwa hatua za malipo. |
| 9.4 | **Shughuli zinazotekelezwa na Mkataba** | a. Kuandaa taarifa za utekelezaji wa Mkataba na kuwasilisha kwenye Sekretarieti ya Mkataba kila baada ya miaka miwili.<br>b. Kuratibu utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Utekelezaji wa Mkataba (NIP, 2018 - 2026).<br>c. Kutekeleza shughuli wezeshi na miradi mbalimbali ambayo ni pamoja na:<br>i. Kuhamasisha Mbinu Bora za Kupunguza Uzalishaji wa Kemikali zinazodumu kwenye Mazingira kwa Muda Mrefu Utokanao na Uchomaji Taka (uPOPs);<br>ii. Uondoshaji wa mafuta yenye kemikali aina ya Polychlorinated biphenyls (PCBs) yaliyopo kwenye transfoma katika nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika) ifikapo 2025;<br>iii. Kuboresha afya na mazingira kwa kuanzisha kituo jumuishi cha ukusanyaji wa taarifa za kemikali na kujengea uwezo taasisi zinazoshughulika na kemikali (African ChemObs); na<br>iv. Mradi wa kuondosha (Decontamination) kemikali katika udongo uliochafuliwa na kemikali zinazodumu kwenye mazingira kwa muda mrefu (Contaminated soil) katika eneo la National Housing Morogoro. |
| 9.5 | | i) Kushiriki kwenye vikao vya Kikanda ambapo nchi wanachama hupata nafasi ya kukutana, kujadili masuala muhimu ya Mkataba, kuainisha vipaumbele na changamoto |

| | | |
|---|---|---|
| | | za kikanda kwa ajili ya kuziwasilisha kwenye vikao vya nchi wanachama;<br>ii) Kushiriki kwenye Mikutano ya nchi wanachama wa Mkataba wa Stockholm ambapo nchi hupata nafasi ya kuchangia Msimamo wa masuala ya udhibiti wa kemikali zinazodumu kwenye mazingira kwa muda mrefu kulingana na Agenda zinazobainishwa. Mkutano wa mwisho Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kushiriki ulifanyika mwezi Mei, 2023 ambapo pamoja na masuala mengine ni pamoja na kuweka makubaliano ya kuondosha baadhi ya kemikali hatarishi na hivyo kuharakisha hatua za kufikia lengo la mkataba wa kulinda afya ya binadamu na mazingira. |
| 9.6 | **Mafanikio** | a. Kuandaliwa kwa Mpango wa Taifa wa Utekelezaji wa Mkataba husika;<br>b. Upatikanaji wa fedha kupitia miradi inayotekelezwa hapa nchini;<br>c. Kusitishwa au kuondoshwa katika matumizi baadhi ya kemikali hatari. Mfano, Dichloro diphenyl trichloroethane (DDT) na Lindane zimeshasitishwa matumizi kwenye kilimo nchini;<br>d. Kudhibiti uingizaji wa kemikali hatari nchini. Mfano, DDT inaruhusiwa kuingizwa kwa kibali maalumu na kwa matumizi mahsusi pekee, ambayo ni kupambana na ugonjwa wa malaria.<br>e. Kuimarisha ushirikiano baina ya nchi na jumuiya ya kimataifa katika nyanja za utafiti na uendelezaji wa teknolojia za kudhibiti kemikali zinazodumu kwenye mazingira kwa muda mrefu;<br>f. Utekelezaji wa miradi ya usimamizi wa kemikali na taka nchini;<br>g. Kuongeza uelewa kwa jamii kuhusu kemikali na taka; na<br>a. Upatikanaji wa fursa za kimasomo katika kozi za usimamizi wa kemikali kwa wanafunzi wa ngazi mbalimbali kupitia miradi. |
| 9.7 | **Changamoto** | b. Uelewa mdogo wa jamii kuhusu kemikali zinazodumu kwenye mazingira kwa muda mrefu<br>c. Kutowasilishwa kwa taarifa za utekelezaji wa matakwa ya Mkataba kutoka katika Taasisi na Sekta kwa mujibu wa majukumu yaliyoainishwa katika Mpango wa Taifa wa |

| | | |
|---|---|---|
| | | utekelezaji wa Mkataba. |
| 9.8 | **Hatua inayofuata** | i) Kuendelea kuratibu utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Utekelezaji wa Mkataba wa Stockholm (NIP, 2018 - 2026) ikiwa ni pamoja na kuibua miradi/shughuli wezeshi katika kutatua changamoto za kemikali zinazodumu kwenye mazingira kwa muda mrefu.<br>ii) Kuendelea kuratibu shughuli zinazotekelezwa chini ya Mkataba ikiwa ni pamoja na kuimarisha uwezo wa kitaasisi na wadau wa sekta mbalimbali katika udhibiti wa kemikali hususan zinazodumu kwenye mazingira kwa muda mrefu kupitia miradi na shughuli wezeshi.<br>iii) Uandaaji wa taarifa za Mkataba, maandalizi na ushiriki katika Mikutano ya Kikanda na ya Nchi Wanachama (Pre-CPP & COP).<br>iv) Kuendelea kutoa Elimu kuhusu madhara ya kemikali zinazodumu kwenye mazingira kwa muda mrefu |
| **10 MKATABA WA BAMAKO KUHUSU UDHIBITI WA TAKA HATARISHI BARA LA AFRIKA** | | |
| 10.1 | Utangulizi | Tanzania ni Nchi mwanachama wa Mkataba wa BAMAKO kuhusu Uzuiaji wa uingizaji wa taka za sumu barani Afrika na kudhibiti usimamizi wake.<br><br>Mkataba huu ni wa kikanda ambao una lengo la kupiga marufuku uingizaji wa taka hatarishi Barani Afrika kwa sababu zozote zile. Tanzania iliridhia Mkataba huu tarehe 15 Februari, 1993.<br><br>Mpaka sasa nchi 29 kati ya 54 za bara la Afrika zimeridhia Mkataba huu<br><br>Majukumu mengine ya Mkataba kwa wanachama wa mikataba ni pamoja na kupiga marufuku uingizaji wa bidhaa na teknolojia za taka hatarishi kutoka nje ya nchi; utupaji wa taka; na kudhibiti biashara ya taka hatarishi ndani ya Afrika au usafirishaji nje ya Africa.<br><br>Wanachama katika mkataba huu pia wanalazimika kushiriki katika usimamizi wa utupaji wa taka hatari zinazozalishwa |

| | | |
|---|---|---|
| | | ndani ya nchi zao. |
| 10.2 | Lengo la Mkataba | Lengo ni kudhibiti wa taka hatarishi zinazovuka mipaka na ndani ya bara la Africa |
| 10.3 | Shughuli zinazotekelezwa na Mkataba | Shughuli zinazofanyika ni pamoja na vikao vya nchi wanachama wa Mkataba wa Bamako vinavyofanyika ila baada ya miaka miwili (2) ambapo mkutano wa tatu (COP 3) ulifanyika mwezi Februari, 2020. |
| 10.4 | Ushiriki wa Mikutano | a. Mkutano wa nchi wanachama wa Mkataba wa Bamako (COP) ambayo hufanyika kila baada ya miaka miwili. |
| 10.5 | Mafanikio | b. Nchi za Afrika kuhakikisha zinazuia uingizaji wa taka hatarishi kwenye Bara la Afrika na hivyo kulinda afya za jamii na mazingira |
| 10.6 | Changamoto | c. Tovuti ya Mkataba inakosa taarifa nyingi na kusababisha ugumu wa kupata taarifa kuhusu Mkataba nan chi wanachama kwa ujumla. Mfano, hakuna sehemu ya kupata taarifa za michango ya nchi.<br>d. Mawasiliano hafifu baina ya Sekretarieti ya Mkataba na nchi wanachama, ikiwemo kupitia tovuti ya Mkataba;<br>e. Kutopatikana kwa taarifa za vikao na mikutano inayopangwa kufanyika au kuhusu kuahirishwa na sababu za kuahirishwa kwake. Mfano, Mkutano wa nne (COP 4) wa nchi wanachama ulipangwa kufanyika mwaka 2022 kwa tarehe ambayo ingetangwaza lakini hakukuwa na taarifa yoyote kuhusu mkutano huo. |

| | | |
|---|---|---|
| **11 MKATABA WA HIFADHI, USIMAMIZI NA UENDELEZAJI WA MAZINGIRA YA BAHARI NA UKANDA WA PWANI YA MAGHARIBI YA BAHARI YA HINDI** | | |
| 11.1 | Utangulizi | Mkataba wa Nairobi Kuhusu Hifadhi, Usimamizi na Uendelezaji wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani ya Magharibi ya Bahari ya Hindi (Convention for the Protection, Management, and Development of the Marine and Coastal Environment of the Eastern African Region) ulipitishwa tarehe 21 Juni, 1985.<br><br>Mkataba huu ulihusisha nchi tisa (9) ambazo ni: Comoro, Kenya, Somalia, Madagascar, Mauritius, Msumbiji, Shelisheli, Re-Union na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tanzania iliridhia Mkataba huu tarehe 1 Machi, 1996. |

| | | |
|---|---|---|
| | | Mwaka 1999 Mkataba huu ulifanyiwa marekebisho ambayo yaliridhiwa na Tanzania tarehe 4 Septemba, 2017. Aidha wakati wa mchakato huo wa marekebisho nchi ya Afrika Kusini ilijiunga kama mwanachama mpya na kufanya idadi ya nchi wanachama kufikia 10. |
| 11.2 | Lengo la Mkataba | Mkataba huu unalengo la kudhibiti uchafuzi wa Mazingira unaotokana na vyanzo na shughuli zinazofanyika nchi kavu. Aidha, Mkataba unalenga Nchi Wanachama, kushirikiana katika kuandaa mipango na mikakati ya pamoja katika kuhifadhi, kusimamia na kuendeleza mazingira ya ukanda wa pwani na bahari. Hii imetokana na dhana ya kuwa bahari ni rasilimali inayochangiwa na nchi zaidi ya moja (transboundary), hivyo juhudi za pamoja ni muhimu katika kusimamia rasilimali zake, ikiwa ni pamoja na kudhibiti uharibifu wa mazingira.<br><br>Aidha, kuongezeka kwa nchi ya Afrika Kusini kama mwanachama mpya kumeongeza wigo wa eneo la Mkataba na kusababisha mabadiliko ya jina la Mkataba kutoka **Mkataba wa Nairobi Kuhusu Hifadhi, Usimamizi na Uendelezaji wa Mazingira ya Bahari na Pwani ya Kanda ya Afrika Mashariki (***Convention for the Protection, Management and Development of the Marine and Coastal Environment of the Eastern African Region*) na kuwa **Mkataba wa Nairobi Kuhusu Hifadhi, Usimamizi na Uendelezaji wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani ya Magharibi ya Bahari ya Hindi** (*Amended Convention for the Protection, Management and Development of the Marine and Coastal Environment of the Western Indian Ocean*). |
| 11.3 | Itifaki zilizopo chini ya Mkataba wa Nairobi | Chini ya Mkataba huu kuna Itifaki ambazo zinaanzishwa kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji wa Mkataba. Itifaki hizo ni pamoja na:<br>*(i)* Itifaki kuhusu Maeneo Tengefu na Wanyamapori na Mimea katika Ukanda wa Afrika Mashariki 1985 (Itifaki hii sasa inarekebishwa - mazungumzo ya mwisho yalifanyika nchini Madagaska mwezi Novemba, 2022) ***"Protocol concerning Protected Areas and Wild Fauna and Flora in the Eastern African Region - 1985" (this is now being amended - last negotiations in Madagascar);***<br>*(ii)* Itifaki ya Usimamizi Shirikishi wa Ukanda wa Pwani katika |

| | | |
|---|---|---|
| | | Kanda ya Magharibi ya Bahari ya Hindi (Rasimu) ***"Protocol on Integrated Coastal Zone Management in Western Indian Ocean Region";***<br>*(iii)* Itifaki inayohusu Ushirikiano katika Kupambana na Uchafuzi wa Bahari katika Matukio ya Dharura katika Ukanda wa Afrika Mashariki1985 ***"Protocol Concerning Co-operation in Combating Marine Pollution in Cases of Emergency in the Eastern African Region - 1985";*** *na*<br>*(iv)* Itifaki ya Udhibiti wa Uchafuzi wa Mazingira ya Bahari na Ukanda wa Pwani ya Magharibi ya Bahari ya Hindi Kutokana na Vyanzo na Shughuli Zinazofanyika Nchi Kavu ***"Protocol for the Protection of the Marine and Coastal Environment of the Western Indian Ocean from Land-Based Sources and Activities - 2010 (LBSA protocol)".*** |
| 11.4 | Hali ya uwasilishaji wa michango ya Nchi | Kila mwaka Tanzania inawajibu wa kuchangia kiasi cha fedha za kimarekeni **45,302** katika Mkataba wa Nairobi. Kwa sasa Tanzania inaidaiwa kiasi cha fedha za kimarekani **631,971** ikiwa ni deni kuanzia mwaka 2004 mpaka 2005 na deni kuanzia mwaka 2011 mpaka 2023. |
| 11.5 | Miradi/shughuli zinazotekelezwa na Mkataba | *(i)* Mradi wa Kufanya tafiti za kijiografia katika maji ya bahari Kaskazini mwa Tanzania ***"Carrying out oceanographic surveys in Northern Tanzania Marine waters"****;*<br>*(ii)* Mradi wa Kuhuisha Utafiti wa Kitaifa wa Uchunguzi wa Mfumo Ikolojia wa Baharini (MEDA) ***"Updating the National Marine Ecosystem Diagnostic Analyses (MEDA)"****;*<br>*(iii) Mradi wa Kuimarisha Mfumo wa Usimamizi Unaozingatia Uhifadhi wa Mazingira kwa lengo la Kuboresha Maisha ya Jamii za Wavuvi katika Wilaya ya Mkinga, Tanzania;* ***"Enhancing Ecosystem-Based Management (EBM) approach for improved livelihood to fisheries communities in Mkinga District, Tanzania – planned"****;*<br>*(iv) Mradi wa Kuimarisha mbinu za kijamii za EBM katika Uvuvi wa Kujikimu na Wadogo kwa Mapato Endelevu na Usimamizi wa Maeneo ya Hifadhi ya Chaneli ya Pemba (PECCA), Zanzibar;* ***"Strengthening community-based EBM approaches in Subsistence and Small-Scale Artisanal Fisheries for Sustainable livelihoods and Management of Pemba Channel Conservation Area (PECCA), Zanzibar";*** |

| | | |
|---|---|---|
| | | *(v)* Mradi wa Utekelezaji wa Programu ya Mpango Mkakati wa Kuzuia uchafuzi wa mazingira ya Bahari Magharibi mwa Bahari ya Hindi kutokana na Shughuli zinazofanyika Nchi kavu Tanzania ***“Implementation of the Strategic Action Programme for the protection of the Western Indian Ocean from land-based sources and activities (WIOSAP) in Tanzania”.***<br>➢ *Uratibu Mkuu na Kufuatilia utekelezaji wa Miradi ya mifano ya programu ya Western Indian Ocean Strategic Action Programme - WIOSAP – VPO* ***“General Coordination and Monitor the implementation of WIOSAP demo Projects – VPO”;***<br>➢ Mradi wa mfano kuhusu njia bora za uhifadhi shirikishi na uvunaji endelevu wa rasilimali za misitu ya mikoko kwenye Delta ya Rufiji, Tanzania ***“Developing collaborative management plan and sustainable mangrove restoration model in Rufiji Delta, Tanzania – UDSM/IMS”****;*<br>➢ Mradi wa mfano wa udhibiti wa maji taka yanayoingia baharini ***“Upscaling and amplification of the Msingini Wastewater treatment facility model in Chake Chake town, Pemba – ZEMA/DOE – ZNZ”****; na*<br>➢ Mradi wa mfano wa usimamizi endelevu wa Mito na Mitiririko yake katika daka maji la Mbalari na Bonde la Rufiji Tanzania ***“Sustainable catchment management through enhanced Environmental Flow Assessment and Implementation for the protection of the Western Indian Ocean form land-based sources and activities in Tanzania – SUA/NEMC”****.* |
| 11.6 | Hali ya ushirikishwaji wa wataalamu nchini | Mkataba umeweza kushirikisha baadhi ya wataalamu hapa nchini katika masuala mbalimbali mbalimbali ya uhifadhi na usimamizi wa mazingira ya rasilimali za bahari na nchi kavu kama ifuatavyo:-<br>(i) Kutayarisha Mkakati wa Kikanda wa Usimamizi wa Taarifa (IMS) unaopendekezwa wa Bahari ya Hindi Magharibi. ***“Developing the proposed regional Information Management Strategy (IMS) for the Western Indian Ocean”;***<br>(ii) Upangaji wa Maeneo ya Baharini (Kikundi Kazi cha Mada) – ***“Marine Spatial Planning - TWG (Thematic Working*** |

| | | |
|---|---|---|
| | | ***Group)";*** *na*<br>(iii) Utawala wa Bahari (Kikundi kazi cha mada) **"Ocean Governance -TWG (Thematic Working Group)".** |
| 11.7 | Mafanikio | i. Upatikanaji wa fedha za kutekeleza miradi mbalimbali kutoka kwenye mfuko wa Sekretarieti ya Mkataba pamoja na wadau wa maendeleo;<br>ii. Kuimarisha ushirikiano wa kikanda na nchi zingine za ukanda wa Magharibi mwa bahari ya hindi katika nyanja ya hifadhi, usimamizi na uendelezaji wa mazingira ya bahari na ukanda wa pwani ya magharibi mwa bahari ya hindi;<br>iii. Kuongeza upatikanaji wa fedha za kigeni kutokana na fedha za miradi zinazoletwa nchini;<br>iv. Utekelezaji wa miradi ya hifadhi ya mazingira ya bahari na ukanda wa pwani ukiwemo mradi wa mfano wa Wilaya ya Mkinga utakaotumiwa na chi zote wanachama wa Mkataba wa Nairobi kujifunza na hivyo kuchangia katika jitihada za maendeleo na upatikanaji wa huduma nchini; na<br>v. Kuongeza uelewa kwa jamii kuhusu uhifadhi wa mazingira ya bahari, faida zake na athari za kutofanya hivyo. |
| 11.8 | Ushiriki wa Mikutano na Matarajio | 11.8.1 Mikutano<br>Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hushiriki katika mikutano chini ya Mkataba wa Nairobi ambayo hufanyika kila mwaka katika ngazi ya Kikanda . Mikutano ambayo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeshiriki katika mwaka 2023 ni pamoja na;-<br>i. Mkutano wa Pili wa Kamati tendaji ya Mradi wa pamoja wa Kikanda baina ya Kamisheni ya Uvuvi ya Ukanda wa Kusini mwa Bahari ya Hindi na Sekretarieti ya Mkataba wa Nairobi uliofanyika kuanzia tarehe 21-22 Mwezi Machi, 2023 Maputo nchini Msumbiji;<br>ii. Mkutano wa Baraza la Mawaziri wa Mazingira wa Afrika (AMCEN) uliofanyika Addis Ababa nchini Ethiopia kuanzia tarehe 14-18 Agosti, 2023;<br>iii. Mkutano wa Pili wa kujadili itifaki ya marekebisho ya maeneo yaliyohifadhiwa ya Flora na Fauna pamoja na kupitisha na kusaini Itifaki ya Usimamizi Jumuishi ya Ukanda wa Pwani (ICZM) katika Kanda ya Afrika |

| | | |
|---|---|---|
| | | Mashariki uliofanyika kuanzia tarehe 11-15 Septemba, 2023 Antananarivo nchini Madagascar;<br>iv. Mkutano/Kikao cha wataalamu na Kamati tendaji ya Mradi wa Mkinga kilichofanyika kuanzia tarehe 02-05 Oktoba, 2023 Tanga, Tanzania;<br>v. Warsha ya Pili ya Afrika kuhusu mpango wa matumizi ya maeneo ya Bahari (Second MSP Forum for Africa), iliyofanyika kuanzia tarehe 05-06 Novemba, 2023 Jijini Dar es Salaam, Tanzania;<br>vi. Kongamano la Pili la Kikanda la Bahari la Mwaka 2023 katika eneo la Magharibi mwa Bahari ya hindi lililofanyika kuanzia tarehe 07-09 Novemba, 2023 Jijini Dar es Salaam, Tanzania;<br>vii. Mafunzo ya Pili ya Kikanda kuhusu Mpango wa Matumizi ya Maeneo ya Bahari yaliyofanyika kuanzia tarehe 20-24 Novemba, 2023 Mombasa, nchini Kenya;<br>viii. Mkutano wa Kikanda wa Kamisheni za Kiuchumi, maafisa viungo pamoja na Jukwaa la Sayansi kwa Sera ulifanyika kuanzia tarehe 04-07 Disemba, 2023 Maputo nchini Msumbiji;<br>ix. Mkutano wa Kikanda wa wataalamu kuhusu mapitio ya viambatisho vya Mkataba wa Basel kuhusu usimamizi wa masuala ya plastiki na kemikali zake kwa ajili ya kujiandaa na usimamizi madhubuti wa Mkataba mpya wa masuala ya Plastiki ulioandaliwa na Sekretarieti za Mikataba wa Nairobi na Basel uliofanyika kuanzia tarehe 11-13 Disemba, 2023 Mahe nchini Seychelles.<br>1.8.2 Fursa na Matarajio<br>i. Upatikanaji wa fedha za kutekeleza miradi kutoka kwa wadau wa maendeleo kupitia Sekretarieti ya Mkataba wa Nairobi;<br>ii. Kujiandaa na majadiliano ya tatu ya itifaki ya marekebisho ya maeneo yaliyohifadhiwa ya Flora na Fauna;<br>iii. Kuimarisha ushirikiano wa kikanda pamoja na Jumuiya za kimataifa katika nyanja ya usimamizi, uhifadhi na uendelezaji wa mazingira ya bahaari pamoja na ukanda wa pwani ya Magharibi mwa Bahari ya Hindi;<br>iv. Kupata ujuzi na kubadilishana uzoefu na wataalamu |

| | | |
|---|---|---|
| | | wengine kutoka nchi za ukanda wa magaharibi mwa bahari ya hindi katika nyanja ya usimamizi, uhifadhi na uendelezaji wa mazingira ya bahaari pamoja na ukanda wa pwani ya Magharibi mwa Bahari ya Hindi;<br>v. Kufuatilia kwa karibu miradi inayotekelezwa chini ya Mkataba wa Nairobi;<br>vi. Kuhakikisha maslahi ya Tanzania yanajumuishwa katika maazimio ya Mikutano ya Kikanda;<br>vii. Kutangaza fursa za uwekezaji kwa wadau mbalimbali kupitia fursa zilizopo katika nyanja ya Uchumi wa Buluu |
| 11.9 | Changamoto | Kupata nafasi chache za ushiriki wa wawakilishi kutoka Tanzania katika Mikutano ya Kikanda inayoandaliwa na Sekretarieti ya Mkataba wa Nairobi. |
| 11.10 | Hatua inayofuata | i. Kujiandaa na Ushiriki wa Mkutano wa nchi wanachama wa Mkataba wa Nairobi (COP 11) unaotarajiwa kufanyika Mwezi Aprili, 2024 nchini Madgascar;<br>ii. Kujenga uwezo na uelewa wa Jamii kuhusu fursa ya biashara ya kaboni kupitia uwepo wa bahari na utunzaji wa mazingira ya bahari hasa miti aina ya mikoko;<br>iii. Kuendelea kushirikiana na nchi wanachama wa Mkataba wa Nairobi katika ukanda wa Magharibi mwa bahari ya hindi katika nyanja ya uhifadhi wa mazingira ya bahari;<br>iv. Kutoa elimu kuhusu biashara ya kaboni (Blue Carbon) kwa wadau wote, wakiwemo wafanya maamuzi, wananchi, wadau wa maendeleo, wanahabari na wawekezaji wa ndani na nje ya nchi ili kuwa na uelewa wa pamoja kuhusu biashara ya Kaboni; na<br>v. Kuendelea kushiriki katika mikutano na majadiliano ya kikanda kwa lengo la kutafuta ufumbuzi wa changamoto za usimamizi na uhifadhi wa mazingira ya bahari na ukanda wa pwani ya magharibi mwa bahari ya hindi. |

| 12 MKATABA WA ROTTERDAM KUHUSU UPASHANAJI TAARIFA KUHUSU BAADHI YA KEMIKALI HATARISHI ZA VIWANDANI NA VIUATILIFU KATIKA BIASHARA YA KIMATAIFA | | |
|---|---|---|
| 12.1 | Utangulizi | Tanzania ni Nchi mwanachama wa Mkataba wa ROTTERDAM kuhusu upashanaji taarifa kuhusu baadhi ya kemikali hatarishi za viwandani na viuatilifu katika biashara ya kimataifa<br><br>Mkataba wa Rotterdam ulipitishwa mwaka 1998 huko Rotterdam (Uholanzi) ambao unalenga kukuza uwajibikaji wa pamoja kuhusiana na biashara ya kimataifa ya kemikali hatarishi. Tanzania iliridhia Mkataba huu mwaka 2004.<br><br>Mkataba huu unasimamiwa na kutekelezwa kwa pamoja na Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA) na Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu (TPHPA).<br><br>Nchi wanachama wa Mkataba zinapaswa kupashana taarifa kuhusu madhara ya kemikali zinazodhibitiwa chini ya Mkataba huu ili kuziwezesha nchi hizo kufanya maamuzi ya kukubali aidha kuziingiza katika nchi husika au kuzisafirisha nje nchi. *(Export and import decisions).*<br><br>Kataba huu umeweka utaratibu kisheria wa kupata ridhaa kutoka nchi mwanachama ambako taka hatarishi inapelekwa au kupitishwa *(Prior Informed Concert – PIC)* |
| 12.2 | Malengo Mahsusi ya Mkataba | Lengo kuu la Mkataba huu ni kuimarisha jitihada za jumuiya ya kimataifa katika kudhibiti uzalishaji na biashara ya kemikali hatarishi kwa ajli ya kulinda afya ya binadamu na mazingira.<br><br>Malengo mahsusi ni pamoja na:<br>i) Kuhakikisha kunakuwepo na uwajibikaji na ushirikiano wa pamoja katika biashara ya Kimataifa kwa baadhi ya kemikali hatarishi na viuwatilifu;<br>ii) Kukuza uwajibikaji wa pamoja katika biashara ya kimataifa ya kemikali hatarishi zenye madhara kwa binadamu na mazingira yake; na<br>iii) Kubadilishana taarifa kuhusu sifa za kemikali ambazo wahusika katika mkataba huu wanafanya biashara ili kuchangia katika matumizi mazuri ya kimazingira ya |

| | | |
|---|---|---|
| | | kemikali hizo. |
| 12.3 | Hali ya Uwasilishaji wa Michango ya nchi | Mkataba huu hauna *Financial Mechanism* |
| 12.4 | Shughuli zinazotekelezwa na Mkataba | Kushiriki Mikutano Kimataifa ya nchi wanachama wa mkataba (COP)<br>Kutekelezwa matakwa ya mkataba ya kutoa ridhaa (Prior Informed Concert) ya kupokea ama kupitisha taka hatarishi pale inapojitikeza |
| 12.5 | Mafanikio | • Ofisi kushiriki katika warsha za kujengewa uwezo kuhusu usimamizi na udhibiti wa kemikali;<br>• Kusaidia kulinda afya ya binadamu na mazingira dhidi ya kemikali zinazodumu kwenye mazingira kwa muda mrefu;<br>• Kuandaa *National Implementation Plan* (NIP) na kuwasilishwa Sekretarieti ya mkataba;<br>• Kupata taarifa kuhusu kemikali hatarishi za viwandani na viuatilifu katika biashara ya kimataifa;<br>• Kuweza kudhibiti kemikali zisizotakiwa kuingizwa nchini; na<br>• Kusaidia kupashana habari kuhusu kemikali hatarishi za viwandani na viuatilifu katika biashara ya kimataifa. |
| 12.6 | Ushiriki wa mikutano | Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hushiriki katika mikutano chini ya Mkataba wa Rotterdam ambayo hufanyika kila baada ya miaka miwili katika ngazi za kimataifa na kikanda. Mikutano ambayo Jamhuri ya Muungano imeshiriki kwa mwaka 2023 ni:<br>• Mkutano wa kikanda uliofanyika Geneva Uswisi; na<br>• Mkutano wa nchi wanachama wa Mkataba uliofanyika Geneva Uswisi. |
| 12.7 | Changamoto | • Usafirishaji haramu wa kemikali hatarishi.<br>• Kukosekana kwa taarifa muhimu kuhusu kemikali zinazosafirishwa nchi mbalimbali. |

| | | |
|---|---|---|
| | | • Baadhi ya nchi kuchelewa au kutokutoa kabisa Idhini ya kupokea taka zinazosafirishwa nje ya nchi.<br>• Baadhi ya nchi kutoridhia au kuchelewa kuridhia baadhi kemikali kuorodheshwa kwenye kiambatisho (Annex) cha kemikali zinazodhibitiwa chini ya Mkataba. |
| 12.8 | Hatua inayofuata | • Kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu maudhui ya Mkataba;<br>• Kuendelea kuratibu ushiriki wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika mikutano ya Kikanda na Nchi wanachama wa Mkataba wa Rotterdam; na<br>• Kuandaa taarifa za kemikali zinazodhibitiwa chini ya Mkataba. |